

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAMLAKA YA MJI MDOGO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji mkuu)



TAREHE 16/07/2021

TANGAZO LA KAZI YA UKUSANYAJI TAKA NGUMU KATIKA ENEO LA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA LOLIONDO.

ZABUNI NAMBA:LGA/005/2021/2022/M/NCS/01 LOT 1

ZABUNI NAMABA:LGA/005/2021/2022/M/NCS/01LOT2

TANGAZO LA ZABUNI.

1. Ofisi ya Mamlaka ya mji mdogo wa Loliondo kwa kuzingatia na kufuata sheria ya usimamizi wa mazingira namba 20 ya mwaka 2004,kifungu cha 117(a) imezitaka mamlaka za serikali za mitaa katika maeneo yao kubainisha njia bora zinazowezezana kwa ukusanyaji wa taka ngumu za aina mbalimbali.."ili kuuweka mji katika hali ya usafi na salama.
2. Afisa mtendaji mkuu wa mamlaka ya mji mdogo loliondo chini ya sheria ya manunuzi ya umma Na.7 ya mwaka 2011 kanuni Na.181 anawatangazia wananchi,makampuni taasisi na vikundi mbalimbali kuomba kazi za uzoaji taka ngumu kama ifuatavyo:

1.UKUSANYAJI TAKA NGUMU ENEO LA WASSO-
LGA/005/2021/2022/M/NCS/01LOT1

2.UKUSANYAJI TAKA NGUMU ENEO LA LOLIONDO NA SAKALA-
LGA/005/2021/2022/M/NCS/01LOT 2


MASHARTI/SIFA MUHIMU ZA MUOMBAJI ZABUNI

- i) Awe Raia wa Tanzania
- ii) Muombaji awe amesajiliwa na mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
- iii) Muombaji awe na uzoefu wa kufanya kazi katika taasisi za serikali
- iv) Muombaji haruhusiwi kuomba kazi zaidi ya moja.
- v)Muombaji aandike barua ya kuomba zabuni ya uzoaji taka na pia aambatanishe leseni ya biashara.
- vi)Muombaji awe na vitendea kazi mfano gari, trekta n.k.

vii) Maombi yanatakiwa kutumwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kuonyesha aina ya zabuni inayo ombwa bila kuwa na viashiria vyovyote inakotoka na yatumwe kwa anuani ifutayo;

KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO,
SLP 1, LOLIONDO

NB. Nyaraka za zabuni zinapatikana katika ofisi ya Mtendaji mkuu wa mji mdogo loliondo, muda na Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **23/7/2021** saa **5.00** asubuhi na zabuni zitafunguliwa saa **5.30** asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Waombaji au Wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi.


Benezeth B. Bwalya
AFISA MTENDAJI MKUU
MJI WA LOLIONDO

**MTENDAJI MKUU
AFISA WA MJI MDOGO
LOLIONDO**